# PRE-MOCK

*Kenya Certificate of Secondary Education (K.C.S.E)*

**KARATASI YA 3**
**FASIHI**
**MUDA: 2 ½**

**Jina** ______________________ **Nambari** ________________

**Sahihi ya mtahiniwa** ________________

**Tarehe** ______________________

**MAAGIZO**

(a) **Jibu maswali manne pekee.**

(b) **Swali la kwanza ni la lazima.**

(c) **Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki.**

(d) **Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.**

for free past papers visit : www.freekcsepastpapers.com

**SEHEMU YA A**

1. **(LAZIMA)** **USHAIRI**

***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali:***

1. Nina hiari kwa ari, kukariri, vizuri hili shairi,
Niwatambulie siri, nibashiri, haya dhahiri shahiri,
Subira yavuta heri, msubiri, niambie kwa umahiri,
Shairi la mashauri, nikariri, busara ni utajiri.

2. Tenda wema kwa hiari, na kwa ari, yote yatakuwa shwari,

Utakuwa mshuhuri, na hodari, tabasamu 'tashamiri,
Yalotendwa kwa hiari, hunawiri, hadi mwisho wa dahari,
Shairi la mashauri, nikariri, busara ni utajiri.

3. Imani na desturi, ni hiari, iwepo 'tazihitri',
Iwe kutoa mahari, kutahiri, lakini ujihadhari,
Usiteme ya sukari, na mazuri, urambe yalo shubiri,
Shairi la mashauri, nikariri, busara ni utajiri.

4. Ninakupa mashauri, sighairi, siwe mwenye taksiri,
Matajiri mashuhuri, askari, na hata maaktari,
Majivuno huaziri, tahayuri, ndo malipo ya kiburi,
Shairi la mashauri, nikariri, busara ni utajiri.

5. Kutoka alfajiri, adhuhuri, alasiri na nadhari,
Japo taweka nadhiri, tafakari, tafadhali tahadhari,
Lazima uwe tayari, na ni heri, utimize kwa hiari,
Shairi la mashauri, nikariri, busara ni utajiri.

6. Maisha kama bahari, ni hatari, yabidi uwe jasiri,
Katu hakuna ya heri, yasoshari, kwa yote uwe tayari,
Hadhari yasikwathiri, tahadhari, kabla yake athari,
Shairi la mashauri, nikariri, busara ni utajiri.

7. Nyenyekea kwa jabari, sighairi, hekima 'furike furi,
Siwe kama msafiri, ni kafiri, msimamo hadhihiri,
Leo hebu stakiri, tabasuri, sidharau mashauri.
Shairi la mashauri, nikariri, busara ni utajiri.

for free past papers visit : www.freekcsepastpapers.com

***Maswali***

(a) Lipe shiari hili kichwa mwafaka. (alama 1 )

(b) Shairi hili ni la bahari gani? Toa sababu ya jibu lako. ( alama 2)

(c) Eleza dhamira ya mtunzi wa shairi hili. (alama 2)

(d) Thibitisha kwamba shairi hili ni la arudhi. ( alama 4 )

(e) Fafanua mashauri manne yanayoangaziwa na mtunzi wa shairi hili. ( alama 4 )

(f) Nakili mwandamizi wa mleo katika ubeti wa tano. ( alama 1 )

(g) Tambua mbinu mbili za lugha zinazotumika katika shairi. Toa mifano. ( alama 2 )

(h) Eleza matumizi ya idhini ya mshairi katika shairi hili. ( alama 2 )

(i) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi. ( alama 2)

(i) Ari

(ii) Umahiri

**SEHEMU B: RIWAYA**

**Kidagaa kimemwozea**

**Ken Walibora**

**Jibu swali la 2 au 3**

2. Angewezaje kumwambia kwamba …… walikuwa katika ukalifu tangu Amani kutiwa mbaroni?
   a. Eleza muktadha wa dondoo hili? (alama 4)
   b. Fafanua sifa **nane** hasi za mzungumziwa (alama 8)
   c. Toa mifano **minane** ya maudhui ya ukatili katika Riwaya ya Kidagaa Kimemwozea(ala 8)

3. Riwaya ya kidagaa kimemwozea inaonyesha jitihada za vijana kujenga jamii mpya.

for free past papers visit : www.freekcsepastpapers.com

Thibitisha kwa kutoa mifano **kumi.** (alama 20)

**SEHEMU C: FASIHI SIMULIZI** **Jibu swali la 4 au 5**

4. a) Eleza maana ya: (alama 4)

   i) ulumbi

   ii) soga

   b) Eleza umuhimu wa soga katika jamii yenu. (alama 4)

   c) Fafanua sifa **nane** bainifu za mlumbi bora (alama 8)

**au**

5. a) Maghani ni nini? (alama 2)

   b) Eleza aina zifuatazo za maghani? (alama 8)

   i) Tondozi
   ii) Sifo
   iii) Tendi
   iv) Rara

   c) Fafanua sifa **sita** za maghani. (alama 6)

   d) Eleza majukumu **manne** ya maghani. (alama 4)

6. **SEHEMU D: HADITHI FUPI**
   **TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINEZO**
   **Shogake dada ana ndevu Alifa Chokocho**

Jadili sifa **kumi** za Safia (alama 20)

7. **SEHEMU E: TAMTHILIA- KIGOGO**

Fafanua kwa kina matatizo **kumi** yaliyowakumba Wanasagamoyo (alama 20)

for free past papers visit : www.freekcsepastpapers.com